



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa Huduma za Mpito katika Elimu Maalum: Mwongozo wa Mzazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuelewa Huduma za Mpito katika Elimu Maalum: Mwongozo wa Mzazi

Huduma za mpito ni seti iliyoratibiwa ya shughuli iliyoundwa kusaidia wanafunzi wenye ulemavu kusonga vizuri kutoka shuleni hadi maisha baada ya shule ya upili. Hii inaweza kujumuisha elimu zaidi, ajira, na maisha ya kujitegemea. Huduma hizi ni sehemu ya Mpango wa Elimu ya Mwanafunzi Binafsi (IEP).

Huduma za mpito huanza lini?

Chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (IDEA), upangaji wa huduma za mpito lazima uanze kufikia umri wa miaka 16 (au mdogo zaidi ikiwa inafaa) katika IEP. Hata hivyo, majimbo mengi huhimiza shule kuanza huduma hizo mapema, kama umri wa miaka 14.

Lengo la kupanga huduma za mpito ni nini?

Lengoni kuwaandaa wanafunzi wenye ulemavu kwa maisha ya baada ya shule ya upili. Hii inajumuisha:

- Elimu baada ya sekondari au mafunzo ya ufundi
- Uajiri (ushindani au kuungwa mkono)
- Kuishi kwa kujitegemea ama kusaidiwa
- Kujihusisha ja jamii na huduma za watu wazima

Ni nani anayehusika katika mchakato wa huduma za mpito?

Kupanga huduma za mpito ni juhudi ya timu. Kwa kawaida inajumuisha:

- Wazazi na walezi
- Waalimu wa elimu maalum na elimu ya ujumla
- Washauri wa shule ama waratibu wa mpito
- Wasimamizi wa shule





- Wawakilishi kutoka kwa jumuiya au mashirika ya huduma ya watu wazima (inapofaa)
- Muhimu sana, mwanafunzi kama mtoa maamuzi mkuu

Ni nini kinachojumuishwa katika mpango wa mpito?

Mpango wa mpito ni ni sehemu ya IEP na lazima ujumuishe:

- Malengo ya baada ya sekondari kulingana na tathmini zinazolingana na umri katika maeneo kama vile elimu, mafunzo, ajira na maisha ya kujitegemea
- Huduma za mpito na shughuli zinazomsaidia mwanafunzi kufikia malengo hayo.
- Kozi ya masomo—seti iliyoratibiwa ya madarasa au uzoefu unaohusishwa na malengo ya mwanafunzi

Ni aina gani za huduma au usaidizi zinazotambuliwa kama huduma za mpito? Mifano ya huduma za mpito hujumuisha:

- Uchunguzi wa kazi na ujifunzaji wa msingi wa kazi (k.m., mafunzo ya kazi au kujifunza kazi kwa kufuatilia anavyofanya kazi mwenzako)
- Mafunzo ya stadi za maisha (k.m., kupika, kupanga bajeti au kutumia usafiri wa umma)
- Usaidizi wa kuweka maombi ya chuo au programu ya ufundi Mahojiano na ujuzi wa kuandika taarifa kuhusu ujuzi wako wa kazi
- Kujifunza jinsi ya kujitetea
- Kuunganishwa na mashirika ya huduma ya watu wazima (k.m., ukarabati wa ufundi)

Wazazi wako na jukumu gani katika kupanga huduma za mpito?

Wazazi ni washirika wakuu katika mchakato. Unaweza :





- Msaidie mtoto wako kugundua uwezo wake, mambo anayopenda kuyafanya na malengo yake ya siku zijazo
- Itisha huduma zinazochangia malengo hayo
- Msaidie mtoto wako kuwa na uzoefu wa maisha halisi (k.m., kazi za nyumbani, kupata kazi, kujitolea kwa kazi za bure)
- Shirikiana na wafanyikazi wa shule na mashirika ya nje

Kuna usaidizi baada ya shule ya sekondari?

Mara tu mwanafunzi anapotoka shule ya upili, ulinzi na huduma chini ya IDEA huisha. Hata hivyo, programu nyinginezo za watu wazima—kama vile Urekebishaji wa Ufundi Stadi (VR) au Huduma za Ulemavu wa Maendeleo (DD)—zinaweza kutoa usaidizi unaoendelea.

Je, Iwapo mtoto wangu hapangi kuhudhuria chuo kikuu?

Mpango wa mpito unapaswa kuonyesha uwezo na mapendeleo ya mtoto wako binafsi, hata kama inahusisha:

- Kuajiriwa na usaidizi
- Shule ya biashara
- Programu za kijamii za siku
- Kuishi kwa kujitegemea au kwa msaada
- Kazi ya kujitolea au shughuli zingine za maana

Nifanyeje sasa kama mzazi?

Hizi ni hatua ambazo unaweza kuchukua:

- Uliza timu yako ya IEP wakati mipango ya mpito itakapoanza (au uombe ianze mapema)
- Mhimize mtoto wako kushiriki katika mikutano ya IEP
- Gundua ujuzi wa kazi na stadi za maisha za mtoto wako ukiwa naye nyumbani





- Jifunze kuhusu huduma za watu wazima na rasilimali za kijamii
- Jihusishe na ujifahamishe----ni safari

Upangaji wa mpito unahusu kumwezesha mtoto wako kujenga maisha yenye maana ya utu uzima. Unapoanza mapema, ndivyo watakavyokuwa tayari zaidi.

Je, naweza kupata usaidizi na mpito nje ya shule kwa lugha yangu?

Mashirika ya huduma za kijamii kawaida hutoa huduma za lugha. Uliza jinsi utakavyomuitisha mkalimani.

Unaweza pia kumwomba kiongozi wa timu ya IEP kuwaalika wawakilishi kutoka wakala wa huduma za kijamii ambao unaweza kushirikiana nao siku zijazo. Mkalimani katika mkutano wa IEP anaweza kusaidia katika mawasiliano.

